JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

MKUU WA TAKUKURU MKOA,
S.L.P 629,
NJOMBE
SIMU (025) 0262782777
Barua pepe:rbcnjombe@pccb.go.tz
Tovuti: www.pccb.go.tz

NJOMBE- 5 JULAI, 2019

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

TAKUKURU MKOA WA NJOMBE YAFUATILIA NA KUKAGUA MIRADI YENYE THAMANI YA SHILINGI BILIONI 20.4

UTANGULIZI

TAKUKURU Mkoa wa Njombe imeendelea kutimiza majukumu yake kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007. Majukumu hayo ni Kuzuia, Kupambana na Kuelimisha. Katika kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni mwaka 2019 TAKUKURU Mkoa wa Njiombe imefanya kazi zifuatazo;

1. **Ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo**

TAKUKURU (M) Njombe imeweza kufuatilia na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo kwa lengo la kuhakiki ubora na thamani ya fedha za umma. Aidha ufuatiliaji huu ulijikita katika ufuatiliaji wa miradi ya afya, maji na elimu. Miradi hii ina thamani ya shilingi bilioni 20.4.

Madhumuni ya Ufuatiliaji

TAKUKURU katika kufanya ufuatiliaji ililenga kubaini endapo fedha na rasilimali nyingine zinazotolewa na Serikali kwa ajili kutekeleza miradi mbalimbali kama inaendana na thamani ya mradi (Value for money), uvujaji (leakage) wa fedha au rasilimali vifaa, kuona kama mradi unawanufaisha walengwa.

Yafuatayo ni mambo muhimu yaliyodhaniwa na kusababisha kufanyika kwa ufuatiliaji wa fedha za miradi ya maendeleo.

i. Kubaini mianya ya Rushwa katika utekelezaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo,

ii. Kujenga uelewa wa pamoja kuhusu kiasi cha fedha kilichotengwa na kutumwa kwa ajili ya

Utekelezaji miradi inayofuatiliwa,

iii. Kuimarisha uwiano kati ya matumizi ya fedha za umma na ubora wa huduma zinazotolewa.

iv. Kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika mchakato wa utekelezaji wa bajeti.

v. Kuimarisha ufanisi na matokeo mazuri ya matumizi ya fedha za umma.

vi. Kubaini mianya ya rushwa na kuchukua hatua kwa wakati kwa mujibu wa majukumu ya kimsingi ya TAKUKURU.

Orodha ya miradi iliyofuatiliwa na kukaguliwa ni kama ifuatavyo.

1. Mradi wa ujenzi wa jengo la mama na mtoto Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa

Mradi huu una thamani ya shilingi milioni mia tano (500,000,000/=) na unatekelezwa kupitia mfumo wa force akaunti. Fedha hizi zinatarajia kujenga na kukamilisha pia jengo la upasuaji, chumba cha kuhifadhia maiti, maabara, kizimba cha kuchomea taka na nyumba moja ya mtumishi. Baada ya ufuatiliaji ilibainika kuwa fedha ambazo zimebakia ni jumla ya shilingi milioni sabini na saba laki sita thelethini na mbiili elfu na mia nne sitini na sita (77, 632, 466.74)

Kilichobainika katika ufuatiliaji wa mradi huu

TAMISEMI ilitoa mwongozo wa matumizi ya fedha zilizopelekwa katika vituo vya kutolea huduma ya Afya nchini, ambapo katika mwongozo huo ulielekeza njia ya manunuzi inayopaswa kutumika kuwa ni “Force Account”, kuwepo kwa kamati za usimamizi wa utekelezaji wa mradi, muundo wa Kamati hizo pamoja na utunzaji wa nyaraka za mradi.

(i) Aidha ufuatiliaji huu umebaini ya kwamba katika **uundaji kamati haukuzingatia muongozo** toka TAMISEMI kwa kuwa kamati zilizoundwa hazikuwa na wataalamu.

(ii) Ufuatiliaji umebaini kuwa **kamati ya manunuzi haikushirikishwa** katika manunuzi ya vifaa vya ujenzi toka viwandani na kwamba manunuzi yote yalifanywa na Afisa Manunuzi Halmashauri ya wilaya Ludewa kitendo kilichopelekea kununua vifaa zaidi ya mahitaji na kuathiri bajeti. Vifaa ambavyo vimenunuliwa zaidi ya mahitaji ni mifuko ya saruji 360 na bati 111. Pia baadhi ya wajumbe wa kamati ya manunuzi kujitoa na kutokushiriki kwenye majukumu yao ya kamati kwa kuona hawakuwa na umuhimu kwenye kamati tajwa.

(iii)Ufuatiliaji umebaini kuwa katika kiasi kilichopokelewa cha shilingi milioni mia tano (500,000,000/=) kiasi cha fedha kilichobaki ni shilingi milioni sabini na saba laki sita thelethini na mbili elfu na mia nne sitini na sita (77, 632, 466.74) na mradi unaendelea kwa utekelezaji. Kazi zilizobaki kukamilisha mradi ni

- ✓ Ujenzi wa jengo la mtumishi kuweka milango, madirisha (Alminium windows), mfumo wa maji, umeme na masinki ya vyoo.
- ✓ Jengo la kuhifadhia maiti kazi zilizobaki ni kuweka milango, madirisha (Alminium windows), mfumo wa maji, umeme na masinki ya vyoo.
- ✓ Maabara kazi zilizobaki ni kuweka milango, madirisha (Alminium windows), mfumo wa maji na masinki ya vyoo.

- ✓ Jengo la mama na mtoto zilizobaki ni kuweka marumaru, rangi, milango, madirisha, mfumo wa maji.
- ✓ Jengo la upasuaji zilizobaki ni kuweka epox, marumaru, rangi, milango, madirisha, mfumo wa maji.
- ✓ Kichomea taka utekelezaji wake bado kwa kuwa fundi aliyekuwa anafajenga amefariki, fedha aliyolipwa ni Tshs. 2,500,000/=

Mapendekezo yaliotolewa

(i) Kamati ya usimamizi wa mradi wa ujenzi wa kituo cha Afya Luilo ihakikishe inakaa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya Ludewa na kuona namna ya kubadilisha matumizi ya vifaa vilivyozidi ambavyo kwa sasa havihitajiki katika mradi ili kuweza kupata vifaa au huduma zinazohitajika katika mradi ili mradi ukamilike na uwe na tija kwa jamii.

(ii) Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Wilaya ya Ludewa ahakikishe kuwa wataalam kutoka ofisi yake wanafanya ukaguzi wa mara kwa mara wakati wa utekelezaji wa miradi akiwemo Mkaguzi wa Mahesabu wa Ndani (Internal Auditor) ili awe anawajengea uwezo wa namna ya kukagua na kutunza nyaraka za mradi vizuri ili fedha ya Serikali isipotee.

2. Mradi wa ujenzi na ukarabati wa shule ya sekondari Mundindi - Ludewa

Mradi huu una thamani ya shilingi milioni mia mbili na hamsini na tisa (259,000,000/=) ambazo mgawanyo wake ni kama ufuatao.

1. Kujenga bweni la wavulana na wasichana likiwa na dari na vitanda shilingi milioni mia moja na hamsini (150,000,000/=)
2. Kujenga madarasa manne yakiwa na dari na madawati shilingi milioni themanini (80,000,000/=)
3. Kujenga matundu kumi ya choo kwa ajili ya wavulana na wasichana na matundu mawili kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum na shilingi milioni kumi na moja (11,000,000/=)
4. Kujenga maabara shilingi milioni kumi na nane (18,000,000/=).

Kilichobainika katika ufuatiliaji wa mradi huu.

(i) Ufuatiliaji umebaini kuwa fedha kiasi cha shilingi milioni mia moja na hamsini (150,000,000/=) kilichokuwa kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa mabweni ya shule ya sekondari Mundindi hadi kufikia mwezi Novemba, 2017 kilikuwa kimetumika chote ingawa wa mradi huo haujakamilika. Mfano: hakuna mfumo wa maji, rangi katika bweni la wasichana, mfumo wa umeme katika bweni la wasichana, vitanda havijatimia katika bweni la wasichana, sehemu ya kufulia (Laundry) haijajengwa kwa mabweni yote na vyoo havijakamilika.

(ii) Ufuatiliaji umebaini kuwa katika utekelezaji wa mradi una mapungufu mbalimbali kama ifuatavyo: Mbao zilizotumika kutengenezea milango, madirisha na vitanda hazina ubora, kuta za ndani zimepakwa rangi bila kufanyiwa skimming, dari inavuja kipindi cha mvua.

(iii) Ufuatiliaji umebaini kuwa hakukuwa na ukaguzi wa mara kwa mara kutoka idara ya ujenzi na idara ya elimu wakati wa utekelezaji wa mradi kitendo kilichopelekea mradi kuwa na kiwango kisichoridhisha.

(iv) Ufuatiliaji huu umebaini ya kwamba hakukuwa na kamati ya manunuzi na mapokezi kama ambavyo mongozo ulielekeza na kwamba kazi zote zilikuwa zinafanywa na kamati ya ujenzi na uongozi wa shule kitendo kilichopelekea kukosekana kwa taarifa na mapokezi ya manunuzi mbalimbali yaliyofanyika kwa ajili ya mradi.

(v) Ufuatiliaji umebani ya kwamba kulikuwa na nguvu za wananchi katika kukusanya mawe, mchanga, kuchimba msingi pamoja na michango ya fedha kiasi cha shilingi milioni kumi na nne laki tatu na elfu sitini (14,360,000/=) lakini kamati haikuanisha matumizi ya fedha zilizochangwa na wananchi na matumizi yake.

Mapendekezo yaliyotolewa baada ya ukaguzi

(i) Kamati ya ujenzi Shule ya sekondari Mundindi ihakikishe kwamba wanamrudisha fundi wa mbao aliyetengeza madirisha, milango pamoja na vitanda ili aweke mbao zenye ubora ili kuleta thamani ya mradi.

(ii) Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Wilaya ya Ludewa ahakikishe ya kwamba kazi zilizobaki kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mabweni zinakamilika hususani mifumo ya maji, rangi bweni la wasichana, mifumo ya umeme bweni la wasichana, vitanda katika bweni la wasichana, sehemu ya kufulia (Laundry) ijengwa kwa mabweni yote na vyoo vikamilishwe.

(iii) Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Wilaya ya Ludewa ahakikishe kuwa wataalam kutoka ofisi yake wanafanya ukaguzi wa mara kwa mara wakati wa utekelezaji wa miradi akiwemo Mkaguzi wa Mahesabu wa Ndani (Internal Auditor) ili awe anawajengea uwezo wa namna ya kukagua na kutunza nyaraka za mradi vizuri.

(iv) Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Wilaya ya Ludewa ahakikishe ya kwamba miradi yote inayotekelezwa katika Halmashauri yake kwa njia ya “Force Account” inazingatia miongozo ya uundaji wa kamati za utekelezaji ili kuleta ufanisi.

3. Mradi wa maji katika kijiji na kata ya Tandala wilayani Makete

Mradi huu unatekelezwa katika kijiji na kata ya Tandala wilayani Makete na una thamani ya shilingi milioni mia saba thelathini na tatu na laki sita (733,600,000/=) kutoka Serikali Kuu. Lengo la mradi huu ni kuwawezesha wananchi wa kijiji hicho kupata maji safi na salama kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Mpaka sasa kimekwisha jengwa chanzo cha maji na tangi na ujenzi umefikia 45%.

Kilichobainika katika ufuatiliaji wa mradi huu

(i) Kingo za chanzo cha maji kuwa chini urefu mita $1^1/2$, imeshauriwa kuongeza urefu na kuwa mita 3 ili kuzuia matope na maji yasipite juu wakati wa masika.

(ii) Hakuna uzio hivyo chanzo kujaa takataka na uchafu mwingi.

(iii) Ujenzi wa barabara kuu ya Njombe – Makete kusababisha njia kuu ya kulaza mabomba ya maji kuhamishiwa upande wa pili wa barabara.

Mapendekezo yaliyotolewa

Kwa sababu ujenzi bado unaendelea kuwepo na ufuatiliaji na usimamizi wa karibu wa mhandisi wa maji wa wilaya ya Ludewa ili kuondoa kabisa mapungufu yanayoweza kusababisha mradi kuchelewa kumalizika au kutekelezwa tofauti na viwango kwa mujibu wa michoro.

4. Mradi wa Elimu - Makete

Mradi huu unahusisha ujenzi wa bweni, nyumba ya mwalimu (two in one), vyumba vitatu vya madarasa, matundu sita ya vyoo, bafu milango sita na sehemu ya kufulia mbili ambao unagharimu jumla ya shilingi milioni mia mbili tisini na mbili (292,000,000/=) Mradi huu unatekelezwa katika wilaya ya Makete. Hadi sasa ujenzi umefikia 75%.

Kilichobainika katika ufuatiliaji wa mradi huu.

(i) Mwitikio mdogo wa wananchi kuchangia nguvu kazi zao kama vile kuchangia matofali, mawe, kokoto na kujitolea kusaidiana na mafundi wakati wa ujenzi, kwa sababu fedha za mfuko wa TASAF pekee zisingetosha kukamilisha mradi bila kusaidiwa na nguvu za wananchi.

(ii) Hali ya hewa ya mvua kuwa nyingi kupelekea vifaa vya ujenzi kufika eneo la ujenzi (site) kuwa vigumu na mafundi kushindwa kufanyakazi kwa sababu ya mvua kunyesha muda mrefu kila siku.

Mapendekezo yaliotolewa

Kwa sababu ujenzi bado unaendelea, uwepo wa ufuatiliaji na usimamizi wa karibu katika utekelezaji wa mradi kama ilivyoanza mwanzo hadi mwisho ili kupunguza au kuondoa kabisa dosari zinazoweza kujitokeza kwenye mradi wakati hatua ya umaliziaji ukiendelea.

5. Mradi wa maji mtiririko - Wanging'ombe

Mradi wa maji mtiririko utahudumia vijiji kumi ambavyo ni Malangali, Hanjawanu, Igandu, Kijombe,Wangamuko, Mpanga, Igayi, Mayale, Lyadebwe na Igowi katika Halmashauri ya wilaya ya Wanging'ombe. Mradi huu una thamani ya shilingi bilioni 12,437,407,360.00 Mkandarasi ameshafanya kazi ya kukusanya wataalamu na vifaa eneo la kazi, uchimbaji wa mtaro, ulazaji wa bomba mita 6 na ujenzi wa tangi la ujazo wa cubic meter 150. Mradi ulianza kutekelezwa tarehe 6/ 8/2018 na unatarajiwa kukamilika July 2019.

Kilichobainika katika ufuatiliaji wa mradi huu.

(i) Imebainika Mkandarasi ameshajenga tangi lenye ujazo wa cubic meter 150 na kukamilika kwa asilimia sabini (70%) ila bado halijajaribiwa ili kuona kama liko vizuri pia ujenzi wa msingi wa kunyanyulia tangi juu umeanza kujengwa katika kijiji cha Hanjawanu pamoja na uchimbaji wa mtaro na ulazwaji wa bomba mita sita.

(ii) Imebainika kwamba kazi ambazo bado ni ni ujenzi wa intake (mtego wa maji) , ujenzi wa fensi kuzunguka intake, ujenzi wa vituo 24 vya kuchotea maji, upakwaji wa rangi kwenye matanki ya maji, nyumba ya mlinzi, ufungwaji wa meter katika vituo vya

maji, ujenzi wa chamber, plaster, ujenzi wa muundombinu wa kutibia maji, ujenzi wa fensi kuzunguka matanki, na ulazwaji wa mabomba ya kusambazia maji km 28 na ulazwaji wa bomba kuu km 18.

(iii)Imebainika kwamba mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 6/ 8/2018 na unatarajiwa kukamilika July 2019.

(iv) Mkandarsi hajalipwa malipo yoyote hivyo tulishauri Halmashauri wamlipe kwa wakati ili aweze kuendelea na kazi.

6. Mradi wa Maji Igongwi lot 1 - Halmashauri ya Mji Njombe

Mradi una lengo la kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa (Luvuyo na Madope) - Wilaya ya Ludewa, Kitulila, Njomlole, Luponde, Madobole, Uwemba na Magoda- Halmashauri ya Mji Njombe na una thamani ya shilingi 4,576,673,868/=

Kilichobainika katika ufuatiliaji wa mradi huu.

Mradi huu umetekelezwa kwa 55% tu. Mkandarasi anasubiri kujibiwa maombi yaliyopelekwa ya kubadili bomba za chuma ili yatumike bomba za plastic kutokana na changamoto iliyojitokeza ya kusafirisha mabomba ya chuma kwenda kwenye chanzo cha maji.

Mapendekezo yaliyotolewa

Wizara iyafanyie kazi mapema maombi ya mkandarasi mshauri na ikiwezekana wizara iwatume wataalum wake mapema ili wakajiridhishe na mazingira ya ugumu wa kazi. Kuchelewa kujibu maombi ya mkandarasi mashauri ni wazi kutachelewesha kukamilika kwa mradi huu mara ya pili na hivyo kusababisha gharama kubwa na lengo la mradi huu kutowanufaisha walengwa kwa wakati.

7. Mradi wa Kidegembye - Halmashauri ya Wilaya ya Njombe

Mradi huu wa maji upo katika kijiji cha Kidegembye na una thamani ya shilingi bilioni 1,354,308,864/=

Kilichobainika katika ufuatiliaji wa mradi huu.

(i) Imebainika kwamba kazi zilizofanyika hadi sasa ni ujenzi wa intake (mtego wa maji) (70%), ujenzi wa nyumba ya pampu (80%), ujenzi wa nyumba ya mlinzi (80%), ujenzi wa bomba kuu km 1.85(100%), ujenzi wa bomba za kusambazia maji km 15.15 (70%) ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 100,000(80%), ujenzi wa vituo 20 vya kuchotea maji pamoja na chamber 15.

(ii) Imebainika kwamba kazi ambazo bado ni ujenzi wa fensi kuzunguka intake,uunganishaji wa umeme, uunganishaji wa pampu, ujenzi wa vituo 10, upakwaji wa rangi kwenye tanki la maji,nyumba ya pampu na nyumba ya mlinzi, ufungwaji wa meter katika vituo vya maji, ujenzi wa chamber, plaster, na ujenzi wa fensi..

Mapendekezo yaliyotolewa

Maombi ya fedha ya mkandarasi kulipwa na wizara kwa wakati baada ya kujiridhisha na kazi zilizofanyika kupitia wasimamizi wa mradi huo.

8. Mradi wa maji ya kusukumwa na pampu Nyave - Halmashauri ya Wilaya ya Njombe

Mradi wa maji ya pampu kijiji cha Nyave ulianza kutekelezwa mwaka wa fedha 2017/2018 na una thamani ya shilingi bilioni 322,555,520/=.

Kilichobainika katika ufuatiliaji huu

(i) Imebainika kwamba kazi alizofanya Mkandarasi zote zilikamilika Kwa asilimia 100 kwa mujibu wa mkataba.

(ii) Mifuniko ya chemba ambayo ilikuwa chini ya kiwango ilikataliwa na Mkandarasi Msimamizi hivyo mifuniko hiyo ilibadilishwa na kutengenezwa ya kiwango na ubora unaotakiwa.

(iii) Imebainika kwamba Mkandarasi alilipwa malipo yake yote.

Mapendekezo yaliyotolewa

Kamati za usimamizi wa maji kusimamia mradi huu kwa ukamilifu ili mradi uendelee kuwanufaisha wananchi wanaozungukwa na mradi huu.

9. Miradi ya ujenzi wa zahanati - Halmashauri ya Mji wa Makambako

Miradi hii ipo katika vijiji vya Mtanga, Ibatu, Mkolango, Utengule, Mtulingala, Ikwete, Usetule, Mahongole na Ngamanga. Pia uboreshaji wa jengo la upasuaji la hospitali Halmashauri ya Mji wa Makambako.Miradi hii inagharimu jumla ya shilingi milioni 488,691,039.12 hadi kukamilika kwake.

Kilichobainika katika ufuatiliaji katika miradi hii

(i) Miradi iliyokaguliwa haijakamilika kama ilivyopangwa kutokana na ukosefu wa raslimali fedha.

(ii) Miradi hutekelezwa kwa kutumia bajeti ya Halmashauri ya Mji wa Makambako na nguvu za wananchi na hivyo kuchukua muda mrefu kukamilika.

(iii) Hakuna ushiriki kamilifu kati ya wadau wa msingi (Direct beneficiary) ambao ni wananchi.

(iv) Katika baadhi ya miradi msimamizi wa mradi ambaye ni mhandisi wa mji wa Makambako kutokusimamia kikamilifu na hivyo kutekelezwa chini ya kiwango mfano, zahanati ya kijiji cha Mahongole tofali na mbao pia wametumika mafundi uashi ambao hawana ujuzi wa kutosha.

(v) Kutokuwepo kwa mikataba ya ujenzi kati ya kijiji/serikali na mafundi waliopewa kazi za ujenzi.

Mapendekezo yaliyotolewa

(i) Halmashauri itenge bajeti za utekelezaji wa mradi ili iishe kwa wakati na wananchi kunufaika.

(ii) Kuwepo na ushirikishaji wa wananchi katika utekelezaji wa mradi ili wananchi washiriki kikamilifu katika kuchangia nguvu kazi na kuwa wamiliki wa miradi hii.

(iii) Mapungufu yaliyoainishwa katika ufuatiliaji huu wa miradi ya maendeleo yafanyiwe marekebisho na mhandisi wa mji wa Makambako ili wananchi wanufaike mapema na miradi.

(iv) Viongozi wa maeneo husika ambapo miradi inatekelezwa baada ya kuibuliwa washirikishwe kikamilifu ili kuongeza usimamizi wa miradi inayotekelezwa..

(v) Mkurugenzi wa mji wa Makambako ahakikishe mhandisi wa mji wa Makambako anatimiza wajibu wake kikamilifu kwa kusimamia miradi ya maendeleo ili kupata miradi yenye viwango na endelevu.

(vi) Sehemu miradi inapotekelezwa yawekwe mabango (Sign board) ili kuonesha mradi unaotekelezwa.

Matokeo ya ufuatiliaji huu wa miradi.

Baada ya ufuatiliaji na ukaguzi wa miradi hii ya maendeleo kwa robo hii ya mwisho jumla ya majalada mawili ya uchunguzi yalifunguliwa baada ya kubainika kwa ukiukwaji mkubwa wa sheria za manunuzi ya umma ya mwaka 2011.

Katika suala la utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, TAKUKURU inawataka watendaji wanaosimamia miradi ya maendeleo kutimiza wajibu wao kikamilifu kwani fedha nyingi zinazoelekezwa katika utekelezaji wa miradi hii. Wasiwe sehemu ya hujuma katika miradi kwa kutanguliza maslahi binafsi mbele. Wasishishirikiane na wakandarasi wasio waaminifu kutekeleza kuhujumu miradi. Wananchi ambao ni wanufaika wa miradi hii washiriki kikamilifu katika utekelezaji na wasisite kutoa taarifa pale wanapoona kuna mazingira ya ubadhilifu wa fedha za umma hasa miradi ambayo wananchi hutakiwa kuchangia nguvu kazi au fedha ili kufanikisha mradi husika.

2. Uchunguzi

Aidha katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2019, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Njombe iliendelea kutekeleza kazi za uchunguzi kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007.

Taarifa zilizopokelewa

Kwa kipindi cha miezi mitatu (April- June, 2019) Ofisi za TAKUKURU Mkoa wa Njombe ulipokea jumla ya malalamiko sitini na mbili (62).

S/N	IDARA	IDADI
1.	Ofisi za watendaji wa vijiji na kata	**17**
2.	Mabaraza ya kata	**14**
3.	Halmashauri za Wilaya na Mji,	**12**
4.	Polisi	**6**
5.	Miradi ya Maendeleo	**5**
6	Afya	**3**

7.	Tanesco	**3**
8	Mahakama	**2**
JUMLA		**62**

Malalamiko haya yalifanyiwa kazi kwa njia mabalimbali ikiwemo kufungua majalada, kupeleka malalamiko katika idara husika na kutoa ushauri kwa walalamikaji.

Kesi mpya zilizofunguliwa mahakamani

Aidha kesi mpya nne **(4)** zilifunguliwa katika mahakama za Mkoa wa Njombe na katika kipindi hiki cha robo ya nne, kesi moja imetolewa maamuzi ambapo mshtakiwa alitiwa hatiani kwa kutumikia kifungo cha miaka mitatu au kulipa faini ya laki tano. Mshtakiwa alikuwa ni Mtendaji wa Kijiji cha Itenyi alilipa faini hiyo. Aidha jumla ya kesi **09** zinaendelea kusikilizwa na zipo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji.

Fedha zilizookolewa

Katika robo ya nne, chunguzi zinazoendelea kuhusiana na miradi ya maendeleo, TAKUKURU imeokoa jumla ya shilingi milioni saba laki mbili na themanini elfu **(7, 280, 000/-)** fedha taslimu ambazo zilifanyiwa ubadhilifu katika ujenzi wa zahanati ya Itambo ilioko wilaya ya Wanging'ombe. Fedha hizi zitarejeshwa kwa Mkurugenzi ili ziweze kutumika kukamilisha mradi huo.

3. Chambuzi za mifumo kwa lengo la kuziba mianya ya rushwa

Katika kipindi cha Aprili hadi Juni , 2019, Mkoa wa Njombe umeweza kufanya chambuzi za mifumo na kufanya warsha na wadau mabalimbali kwa lengo la kuziba mianya ya Rushwa katika idara na taasisi za umma. Jumla ya mifumo mitano (5) ilichambuliwa katika maeneo yafuatayo;

(i) Uchambuzi wa mfumo ulifanyika katika matumizi ya fedha za ruzuku kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Halmashauri ya Mji Njombe. Ilibainika kuwa fedha kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum, zimekuwa pia zikitumika kufanya malipo ya shughuli zingine tofauti na lengo lake.

(ii) Uchambuzi wa mfumo ulifanyika pia katika huduma za uunganishaji umeme majumbani. Ilibanika kuwa wakati wa mchakato wa maombi toka kwa wananchi ili kuunganishiwa umeme majumbani kuna mianya ya rushwa ambayo huchangiwa na uhaba wa vifaa vya umeme huku maombi ya wananchi ya kuunganishiwa umeme yakiwa ni mengi.

(iii) Uchambuzi wa mfumo pia ulifanyika katika uendeshaji wa mabaraza ya kata. Ilibainika kuwa wananchi wanaofika kupata huduma za mabaraza ya kata wamekuwa wakitozwa gharama kubwa za ada, gharama kubwa katika kuhamisha baraza kufika eneo lenye mgogoro na kutoa maamuzi kwa kuangalia uwezo wa mtu.

(iv) Uchambuzi pia ulifanyika juu ya ulipaji wa kodi za majengo. Ilibainika kuwa wananchi wengi ukiacha waishio mjini, bado hawana ufahamu wa kutosha kuhusu kodi za majengo zinavyolipwa. Hii inachangia fedha zinazokusanywa kwa njia ya kujaza

fomu na kupeleka fedha kwa watendaji kuacha mwanya kama fedha hizi zinafika serikalini.

(v) Katika kipindi hiki, uchambuzi pia ulifanyika juu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ilibainika kuwa pamoja na lengo jema la Serikali katika kutekeleza miradi mbalimbali, wananchi ambao ni wanufainka hawashirikishwi vya kutosha na hivyo kukosa umiliki wa miradi hii. Hii inaacha mwanya kwa baadhi ya watendaji wanaosimamia miradi hii wasiowaaminifu kujinufaika na fedha za miradi na hivyo kupelekea miradi kutokamilika kwa wakati.

4. Warsha

Katika hatua nyingine, kufuatia kufanyika kwa chambuzi za mifumo, TAKUKURU Mkoa wa Njombe ilifanya jumla ya warsha 3 na wadau kwa lengo la kujadili na hatimaye kuziba mianya ya rushwa katika mifumo ya uendeshaji na utendaji kazi. Warsha zilizofanyika kujadili mapungufu yaliyobainishwa wakati wa chambuzi za mifumo na hatimaye kuweka maazimio ya pamoja ni kama ifuatavyo.

(i) Warsha juu utoaji mikopo kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu katika Halmashauri ya Mji Njombe

(ii) Warsha juu ya uendeshaji wa Mabaraza ya Ardhi Vijiji na Kata katika kata ya Uwemba, Halmashauri ya Mji Njombe.

(iii) Warsha juu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

Kwa lengo la kuziba mianya ya rushwa, maazimio ya pamoja yaliwekwa na wadau na TAKUKURU ilifanya ufuatiliaji (Compliance) ili kuona kama maazimio ya pamoja yaliyowekwa katika warsha yalitekelezwa. Matokeo ya ufuatiliaji wa ilikuwa ka ifuatavyo.

Mikopo kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu

(i) Halmashauri ya mji wa Njombe kwa sasa inatoa taarifa kwa watendaji wa mitaa na vijiji pindi ikiwa tayari kutoa mikopo kwa walengwa

(ii) Watendaji wa mitaa/vijiji wanakaa vikao kila mwisho wa mwezi na moja ya ajenda ni kupitisha maombi ya vikundi kisha maombi hayo kupelekwa kamati ya maendeleo ya kata (KAMAKA)

(iii) Halmashauri ya mji kupitia idara ya maendeleo ya jamii itaendelea kutoa elimu ya ujasiriamali na kwa makundi yanayopewa mikopo.

Mabaraza ya kata

(i) Halmashauri zipo kwenye mchakato wa kuandaa tozo kwa ajili ya mabaraza ya kata pamoja na posho za wajumbe wa mabaraza ya kata.

(ii) Halmashauri zimeanza kutoa semina za kuwajengea uwezo wajumbe wa mabaraza ya kata.

(iii) Elimu kwa wananchi inaendelea kutolewa na halmashauri juu ya uwepo wa mabaraza ya kata, na majukumu yanayotekelezwa na mabaraza. Elimu hii hutolewa kupitia wanasheria wa halmashauri.

(iv) Miongozo ya sheria tayari imekwisha sambazwa kwenye kata na halmashauri ya wilaya ya Ludewa.

5. Uelimishaji umma

TAKUKURU iliendelea na jukumu la kuelimisha umma kwa kutumia njia mbalimbali kwa lengo la kuhamasisha wananchi kushiriki kwa vitendo katika mapambano dhidi ya Rushwa. TAKUKURU iliendesha **semina 11** katika makundi mabalimbali ndani ya mkoa wa Njombe na kufanya **mikutano ya hadhara 27** kwa wananchi. **Vipindi 4 vya radio** vilirushwa vikihamasisha mapambano dhidi ya Rushwa na **taarifa kwa umma 5** zilitolewa kwa wananchi kupitia vyombo vya habari kwa lengo la kuwafahamisha wananchi mambo mabalimbali yaliyofanywa na ofisi za TAKUKURU Mkoa wa Njombe. Katika kuelimisha kundi la vijana jumla ya klabu za wapinga Rushwa 52 zilitembelewa kwa lengo la kuimarishwa na klabu za wapinga Rushwa na klabu 45 zilifunguliwa katika shule za msingi na sekondari.

MAENEO YA KIPAUMBELE 2019/2020

TAKUKURU itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ambayo ni uchunguzi, uelimishaji, utafiti/udhibiti lakini pia itaendelea na jukumu la ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ya kimkakati husani miradi ya elimu, maji na afya na kuendelea kuchambua mifumo ya ukusanyaji kodi na mapato ya Serikali. Kwa kuwa huu ni mwaka wa uchaguzi, TAKUKURU itaendelea kuelimisha umma juu ya madhara ya vitendo vya Rushwa katika chaguzi.

WITO

TAKUKURU inatoa wito kwa watumishi wa umma, wakati wote wa utendaji kazi kuzingatia sheria, kanuni na taratibu kwa mujibu wa majukumu yao ya kazi, wajiepushe na ubadhilifu au wizi wa mali za umma.

TAKUKURU inawashukuru wananchi kwa kuendelea kutupa ushirikiano na kutuamini na tunaomba moyo huo uendelee, wananchi waendelee kutoa taarifa za vitendo vya Rushwa na watumie haki yao kwa mujibu wa katiba ya nchi kuwachagua viongozi watakaosimamia mendeleo yao kwa muda wa miaka mitano.

TAKUKURU inaomba waandishi wa habari kuwa sehemu ya mapambano dhidi ya rushwa kutokana na kazi zenu mnazofanya za kuelemisha jamii. Tunaamini masikio yenu ni marefu sana ya kuweza kusikia kero mabali mbali za wananchi na kuzifikisha TAKUKURU. Pia kupitia vyombo vyenu vya habari tunaomba muendelee kufikisha njumbe mbali mbali za TAKUKURU kwa wananchi.

Imetolewa na

DOMINA MUKAMA
MKUU WA TAKUKURU [M]
NJOMBE

5/7/2019